# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

# MPANGO KABAMBE WA MIFUGO TANZANIA (TANZANIA LIVESTOCK MASTER PLAN) 2017/2018 – 2021/2022

## MUHTASARI

**Wizara ya Mifugo na Uvuvi**
**S.L.P. 2870,**
**40487 DODOMA**

**Desemba, 2017**

## 1. UTANGULIZI

Sekta ya mifugo ni muhimu katika kuwezesha wananchi kupata chakula, kipato, wanyama kazi pamoja na samadi kwa ajili ya kurutubisha ardhi na hivyo kuwezesha ustawishaji wa mazao, hususan maeneo ya vijijini na baadhi ya maeneo ya mijini na pembezoni mwa miji. Kaya takriban milioni 4.6 zinajihusisha na ufugaji, ikiwa ni asilimia 50 ya kaya zote nchini (NPS, 2012). Uwiano wa asilimia ya kipato cha Kaya hizo inayotokana na ufugaji wa mifugo ni kama ifuatavyo:

- Kuku asilimia 53;
- ng'ombe asilimia 32;
- mbuzi asilimia 10;
- nguruwe asilimia 4; na
- kondoo asilimia 1.

Katika mwaka 2016, sekta ya mifugo imekua kwa asilimia 2.6 na kuchangia asilimia 7.4 katika pato la Taifa. Mchango wa sekta bado ni mdogo ukilinganisha na idadi ya mifugo iliyopo ambayo ni ng'ombe milioni 28.4 mbuzi milioni 16.6 na kondoo milioni 5, kuku wa asili milioni 37.4 (NBS, 2016).

Sababu za ukuaji na mchango mdogo wa sekta katika pato la Taifa ni kutokana na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na uzalishaji mdogo; kuongezeka kwa vifo vya mifugo; kuendelea kuenea kwa magonjwa na changamoto za malisho na maji ya mifugo.

Kutokana na changamoto hizo, mwezi Novemba, 2015 Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (International Livestock Research Institute –ILRI) kwa ufadhili wa Taasisi ya Bill & Melinda Gates Foundation (BMGF) ilifanya uchambuzi wa kina na kuanza maandalizi ya Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania (Tanzania Livestock Master Plan – TLMP) ambao ulilenga kufanya tathmini ya kina katika sekta ya mifugo ili kuona nini kifanyike kwa lengo la kuibadili kabisa sekta hii inayotegemewa na watanzania zaidi ya asilimia 50.


## 2. UTAYARISHAJI WA MAENEO YA KIPAUMBELE

Mpango umeandaliwa kwa kutumia Mfumo maalam wa kuchakata taarifa za mifugo ujulikanao kama Livestock Sector Investment and Plolicy Toolkit (LSIPT) kwa kutumia takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu NBS, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wafugaji na wataalam wa mifugo. Mfumo huo maalum ulitumika kwa mara ya kwanza nchini Ethiopia na Tanzania ikawa nchi ya pili barani Afrika kuutumia, ulisaidia kujua hali halisi ya sekta ya mifugo kuhusu ukuaji, uzalishaji, mapato kwa kaya na Taifa. Aidha, kwa kutumia mfumo huo, tathmini ya sekta ya mifugo kwa miaka 15 (Livestock Sector Analysis- LSA) iliwezesha kujua hali ya uzalishaji na mahitaji ya mazao yatokanayo na mifugo kwa miaka 15 ijayo kwa kuzingatia ongezeka la idadi ya watu, ukuaji wa miji na kipato.

Kutokana na tathmini hiyo ilionekana kuwa kwa miaka 15 ijayo (kufikia mwaka 2032) nchi itakumbwa na uhaba mkubwa wa nyama hasa nyama nyekundu kiasi cha tani 1,731,000 sawa na upungufu wa asilimia 33 ya mahitaji. Aidha, kama hakutakuwa na juhudi za ziada za kuongeza uwekezaji katika sekta ya mifugo, Tanzania itakuwa na upungufu mkubwa wa bidhaa zitokanazo na mazao ya mifugo hivyo kulazimika kuagiza kutoka nje ya nchi.

**Makisio ya mahitaji (demand) na ugavi (supply) wa nyama nyekundu nchini kulingana na ukubwa wa uwekezaji, 2017-2032 ni kama ilivyooneka katika graph hapa chini.**

**Makisio ya mahitaji (demand) na ugavi (supply) wa nyama nyekundu nchini kulingana na ukubwa wa uwekezaji, 2017-2032 ni kama ilivyooneka katika graph hapa chini.**




## 3. MALENGO YA MPANGO

Lengo kuu la Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania (TLMP) ni kuleta mageuzi katika mifugo kwa kuzingatia mnyororo wa thamani. TLMP itatekelezwa kwa awamu tatu ya miaka mitano (5) kila moja kwa muda wa miaka 15 kuanzia mwaka 2017/2018 – 2031/2032. Malengo ya TLMP yanazingatia malengo ya kitaifa ambayo ni:

i. Kuchangia katika kuondoa umaskini;
ii. Kuchangia usalama na uhakika wa chakula na lishe;
iii. Kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi;
iv. Kuchangia ongezeko la mapato yatokanayo na mauzo ya nje; na
v. Kuchangia malighafi za viwanda vya kuongeza thamani mazao ya mifugo.

## 4. MAENEO YA MPANGO

Mpango huu umeainisha maeneo ya kimkakati ya uwekezaji kwa ajili ya kuboresha mbari za mifugo (animal breeding); afya ya mifugo; maeneo ya malisho na vyakula vya mifugo; kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na mifugo na masoko; kuimarisha tafiti; mafunzo na huduma za ugani na mapitio ya sera mbalimbali ili kufikia malengo ya Kitaifa yanayolenga kuifanya Tanzania kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, kwa kupitia Programu pana ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo ya awamu ya pili (ASDP II).

## 5. MAZAO YA VIPAUMBELE NA KANDA ZA MIFUGO

Kutokana na matokeo ya uchambuzi wa sekta ya mifugo ili kufikia malengo ya Serikali yaliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha 2016/2017- 2020/2021, TLMP imeainisha uwekezaji wa kuboresha mnyororo wa thamani wa mazao yafuatayo;

i. Nyama nyekundu kutoka kwa ngombe, mbuzi na kondoo kwa kuboresha mifugo ya asili, ranchi na unenepeshaji;
ii. Kuku kwa kuboresha kuku wa asili na wafugwao kibiashara (kuku wa nyama na mayai);
iii. Kuboresha nguruwe wafugwao kwa mfumo wa asili na wa kibiashara;
iv. Ng'ombe wa maziwa katika kaya na mashamba ya kibiashara.
v. Tasnia ya ngozi

Aidha, TLMP imeainisha kanda tatu za mifugo nchini ambazo ni (i) Nyanda za Juu ikijumuisha Kanda ya Kaskazini (Arusha na Kilimanjaro) na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Iringa, Katavi, Mbeya, Njombe, Rukwa na Songwe); (ii) Kanda ya Kati (Dodoma, Manyara, Morogoro, Simiyu, Singida, Tabora na Shinyanga), (iii) Kanda ya Pwani (Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Pwani na Tanga) na Ziwa (Geita, Kagera, Kigoma, Mara na Mwanza).

- Kanda ya Juu imeainishwa kwa ajili ya uwekezaji na uzalishaji wa maziwa kama zao kuu,
- Kanda ya Kati kwa ajili ya uwekezaji na uzalishaji nyama; na
- Kanda ya Pwani na Ziwa kwa ajili ya uwekezaji na uzalishaji wa nyama na maziwa kwa upande wa ng'ombe mbuzi na kondoo.

## 6. MATOKEO YANAYOTARAJIWA NA MIKAKATI ILIYOAINISHWA


Katika kipindi cha miaka mitano (2017/18 - 2021/2022) cha utekelezaji wa TLMP matokeo yatakuwa kama ifuatavyo:

### 6.1 Tasnia ya Maziwa:

- Kuongezeka kwa idadi ya ng'ombe wa maziwa kutoka ng'ombe 782,992 mwaka 2016/2017 hadi 2,985,000 (2021/22; na
- Kuongezeka uzalishaji wa maziwa kutoka lita bilioni 2 hadi lita bilioni 3.8.

Ongezeko la idadi ya ng'ombe wa maziwa litachangia uzalishaji wa maziwa wa kutosheleza viwanda vya ndani na ziada kwa ajili ya kusindika kuwa yenye kuhifadhiwa kwa muda mrefu bila kuhitaji jokofu kama ya unga (powdered milk) na ya kimiminika (Ultra Heat Treated - UHT).


**Makisio ya mahitaji na ugavi wa maziwa nchini kulingana na ukubwa wa uwekezaji, 2017-2032**




### 6.2 Tasnia ya Nyama:

i. Kuongezeka kwa uzalishaji wa nyama nyekundu kutoka tani 394,600 mwaka 2016/17 hadi tani 742,500 mwaka 2021/22.

**Makisio ya mahitaji (demand) na ugavi (supply) wa nyama nyekundu nchini kulingana na ukubwa wa uwekezaji, 2017-2032 ni kama ilivyooneka katika graph.**




### 6.3 Tasnia ya Ngozi

Mkakati wa kuboresha mbari za mifugo, afya ya mifugo, na maeneo ya malisho na vyakula vya mifugo utaongeza idadi ya mifugo iliyo bora na hivyo kuongezeka kwa idadi kubwa ya vipande vya ngozi na ubora wa ngozi kwa ajili ya viwanda vyetu. Hadi sasa viwanda vya ngozi vilivyopo nchini ni 9.

| NA. | JINA LA KIWANDA | MAHALI | UWEZO WA KUSINDIKA -VIPANDE (Feet$^2$) | | HALI HALISI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ng'ombe | Mbuzi/ Kondoo | |
| 1 | Lake Trading Co. Ltd | Kibaha | 90,000 | 420,000 | Kinafanya kazi |
| 2. | Himo Tanneries and Planters | Moshi | 90,000 | 900,000 | Kinafanya kazi |
| 3 | Sak International Ltd | Arusha | 450,000 | 900,000 | Kinafanya kazi |
| 4 | Ace Leather Ltd | Morogoro | 1,200,000 | 3,600,000 | Kinafanya kazi |
| 5 | Salex tanneries Ltd | Arusha | 624,000 | 1,500,000 | Kinafanya kazi |
| 6 | Moshi Leather Industries Ltd | Moshi | 180,000 | 1,200,000 | Kinafanya kazi |
| 7 | Afro Leather Industries | DSM | 300,000 | 700,000 | Hakifanyi kazi |
| 8 | Hua Cheng | Dodoma | 900,000 | 1,500,000 | Hakifanyi kazi |
| 9 | Xing Hua Investment | Shinyanga | 900,000 | 2,100,000 | Hakifanyi kazi |
| | **JUMLA** | | **4,734,000** | **12,820,000** | |

### 6.4 Mazao Mengine ya Mifugo

Mazao mengine ya mifugo yenye umuhimu kiuchumi ni pamoja na pembe, kwato, mifupa, damu na manyoya. Mazao haya yanatumika Kwa njia tofauti tofauti kama kutengeneza vyakula vya mifugo, madawa na mavazi. Uhamasishaji wa uzalishaji endelevu wa mazao haya ni mdogo unaosababishwa na elimu ndogo kuhusu umuhimu wa mazao hayo, ujuzi mdogo wa kuzalisha mazao hayo na ukosefu wa tekinolojia.

Kwa kupitia Mpango Kabambe wa Mifugo Serikali itahamasisha njia sahihi za uzalishaji na utumiaji wa mazao haya; uanzishawji wa viwanda vya kusindika mazao hayo; kusaidia tafiti ya njia nzuri za matumizi ya mazao mengine yatokanayo na mifugo; na kwa kushirikiana na wadau wengine itaimarisha upatikanaji wa taarifa za masoko.

## 7. MASUALA MTAMBUKA

### 7.1 Kudhibiti rasilimali za mifugo

Ili kudhibiti rasilimali za mifugo nchini, mpango utaweka na kusimamia operesheni ya kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali unaosababishwa na utoroshaji wa rasilimali za mifugo nje ya nchi, uingizaji wa bidhaa za mifugo bila kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo na biashara holela ya mazao ya mifugo na pembejeo.

### 7.2 Uwekezaji wa sekta binafsi kwenye kuongeza thamani ya mazao ya mifugo na mazao yatokanayo na mifugo

Serikali ina jukumu la kuweka mazingira bora ili kuchochea sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya mifugo, ili kutatua baadhi ya changamoto kama:

i. Uwepo kwa mamlaka nyingi za Serikali za udhibiti na kusababisha usumbufu usiokuwa wa lazima kwa wawekezaji.
ii. Ushindani usio wa haki unaosababishwa na uingizwaji wa bidhaa za ndani kutoka nje na kusababisha bidhaa kukosa masoko ya uhakika, tozo nyingi kwa baadhi ya bidhaa, pamoja na ukosefu wa umeme wa uhakika kwa ajili ya viwanda.
iii. Kujenga viwanda vya mazao ya mifugo (nyama, maziwa na ngozi) ikiwa ni pamoja na kufufua viwanda vilivyotelekezwa.

### 7.3 Mchango wa Sekta ya Mifugo kwenye Kuongeza Ajira

Kaya zinazomiliki mifugo nchini ni milioni 4.493 ambapo kuku na ng'ombe wanaongoza ukilinganisha na mifugo mingine. Kila kaya inakadiriwa kuwa na watu watano na hivyo kufanya idadi ya watu wanaojihusisha na ufugaji kuwa milioni 22.5 sawa na aslilimia 50 ya watanzani. Sekta ya mifugo ina umuhimu mkubwa katika kujenga uchumi imara, kuongeza kipato na fursa za ajira nchini. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kuendeleza Mifugo nchini awamu ya kwanza inakadiriwa kwamba kutakuwa na ongezeko la ajira ya watu wapatao milioni mbili ambao watakuwa wanajishughulisha na ufugaji.

## 8. UGHARAMIAJI

Mpango huu ni sehemu ya Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya pili (Agricultural Sector Development Programme - ASDP II), hivyo mfumo na vyanzo vya ugharamiaji wa mpango huu umeainishwa kwa kina kwenye ASDP II.

Mpango huu umeainisha uwekezaji wa jumla ya shilingi **bilioni 1,393.9** ambapo Serikali inatarajiwa kuweza shilingi **bilioni 502.6 (36%)** na sekta binafsi shilingi **bilioni 891.3 (64%).**

**Mchanganuo wa jumla ya gharama za uwekezaji za programu ya TLMP**

| Na. | Maeneo ya Uwekezaji | Jumla ya gharama za uwekezaji (TZS) | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Serikali | Sekta Binafsi | Jumla |
| 1 | Ng'ombe wa Maziwa | 105.8 | 119.3 | 225.1 |
| 2 | Nyama/Maziwa na unenepeshaji | 184.8 | 157.4 | 342.2 |
| 3 | Kuku | 195.9 | 557.5 | 753.4 |
| 4 | Nguruwe | 16.1 | 57.1 | 73.2 |

## 9. UFUATILIAJI NA TATHMINI

Ufuatiliaji na tathmini ya TLMP utafuata mfumo wa ufuatiliaji wa Programu ya Kuendeleza Kilimo awamu ya pili (ASDP II) ambao umeainisha viashiria vya sekta ya kilimo (Results framework matrix) vikiwemo viashiria vitakavyopima maendeleo ya Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania.

## 10. MFUMO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO KABAMBE WA MIFUGO TANZANIA (TLMP IMPLEMENTATION FRAMEWORK)

TLMP inatekelezwa kwa mfumo wa utekelezaji wa vipaumele vya sekta ya kilimo kwa upana wake kupitia Programu ya awamu ya pili ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II. Lengo la ASDP II ni kufanya mageuzi

ya sekta ya kilimo kwa ujumla wake (mazao, mifugo na uvuvi) ili kuongeza uzalishaji na tija kwa ajili usalama wa chakula, kuongeza kipato kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na Taifa kwa ujumla.

ASDP II inatekelezwa kwa kuzingatia vipaumbele (focus) vya:

- Mazao machache (Commodity selection);
- Maeneo ya kikanda (Agricultural Ecological Zone/clustering); na
- Mnyororo wa thamani (commodities Value Chain).

Aidha, vipaumbele vilivyoainishwa kwenye TLMP vimeoanishwa na baadhi ya maeneo 23 vya vipaumbele (Priority Investment Areas) vya ASDP II katika maeneo makuu manne (4).

| Maeneo ya ASDP II | Vipaumbele 23 vya ASDP II | Vipaumbele vya TLMP (vinavyolingana na vya ASDP II) |
|---|---|---|
| **Eneo la 1: Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya maji na ardhi** | 1. Mpango maalum wa matumizi ya ardhi na usimamizi wa mwachano (watershed) wa maji;<br>2. Kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji,<br>3. Kuendesha na Kusimamia skimu za umwagiliaji;<br>4. Kuwezesha uendelezaji wa vyanzo vya maji kwa ajili ya mifugo na samaki;<br>5. Kuendeleza teknolojia za kilimo zenye kuhifadhi mazingira na mabadiliko ya tabianchi; | *1. Kuendeleza mipango wa uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya ufugaji (communal grazing land);*<br>*2. Kuendeleza na kuboresha miundombinu ya mifugo ya maji; malisho na nyanda za malisho;*<br>*3. Kuimarisha teknolojia ya uvunaji na uhifadhi ya malisho kutokana na mabadiliko ya tabianchi.* |
| **Eneo la 2: Kuongeza Tija na Faida.** | 1. Kuimarisha huduma za ugani na mafunzo na kuendeleza upatikanaji wa taarifa za kilimo, mifugo na uvuvi;<br>2. Kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora na pembejeo za kilimo, mifugo, uvuvi na huduma za afya;<br>3. Kuendeleza na kuimarisha shughuli za utafiti;<br>4. Kuimarisha na kuendeleza matumizi ya zana bora (mashine na mitambo);<br>5. Kuimarisha Usalama wa chakula na lishe. | *1. Kuimarisha huduma za utafiti, ugani na mafunzo;*<br>*2. Kuongeza upatikanaji na matumizi ya pembejeo na zana za mifugo;*<br>*3. Kuimarisha na kuendeleza teknolojia za uzalishaji wa pembejeo bora za mifugo (AI), malisho bora na uhifadhi;*<br>*4. Kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora, pembejeo na huduma za afya ya mifugo (udhibiti wa magonjwa);*<br>*5. Kuimarisha maabara za mifugo za kukakiki ubora wa pembejeo za mifugo na uzalishaji wa chanjo za mifugo;*<br>*6. Kuendeleza kosaafu bora za mifugo ili kuongeza tija katika uzalishaji wa maziwa, nyama, mayai na wanyama hai.* |
| **Eneo la 3: Biashara na Kuongeza Thamani ya Mazao** | 1. Kuendeleza upatikanaji wa masoko na mifumo ya masoko kwa ajili ya mazao yote ya kipaumbele;<br>2. Kuendeleza upatikanaji wa masoko na mifumo ya masoko kwa ajili ya mifugo, uvuvi na bidhaa zake; | *1. Kuboresha upatikanaji wa masoko na kuongeza thamani ya mazao ya mifugo;*<br>*2. Kuimarisha uwezo wa taasisi na mifumo ya taarifa kwa ajili ya maendeleo na usimamizi wa sekta za mifugo;* |

| Maeneo ya ASDP II | Vipaumbele 23 vya ASDP II | Vipaumbele vya TLMP (vinavyolingana na vya ASDP II) |
|---|---|---|
| | 3. Kuendeleza usindikaji na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. | *3. Kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya kukuza uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta ya mifugo.* |
| **Eneo la 4: Kuiwezesha Sekta katika Uratibu, Ufuatiliaji na** | 1. Kupitia na kuboresha sera, miongozo na pia kuboresha mazingira ya biashara za kilimo, mifugo na uvuvi;<br>2. Kuimarisha miundo na uwezo wa kitalaam wa vikundi vya wakulima na/ au vyama vya wazalishaji, wafanyabiashara, na wasindikaji wadogo;<br>3. Kuanzisha na kuendeleza ushiriki wa makundi/jinsia tofauti kwenye sekta ya Kilimo;<br>4. Kuimarisha uratibu wa sekta katika ngazi zote za utekelezaji;<br>5. Kuwezesha upatikanaji na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa takwimu katika sekta ya kilimo;<br>6. Kuimarisha uwezo na mifumo ya uongozi katika sekta ya kilimo;<br>7. Kuandaa na kuimarisha Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini;<br>8. Kuwezesha na kuimarisha uwezo wa utendaji wa shughuli za kilimo kwa watendaji wa sekta ya kilimo katika ngazi zote;<br>9. Kuimarisha mifumo ya kiteknolojia ya habari na mawasiliano katika sekta ya kilimo (TEHAMA);<br>10. Kutoa na kuwezesha huduma za kifedha (daraja la kawaida katika kuendeleza shughuli za kilimo (provide microfinance services). | *1. Kupitia na kuboresha sera, sheria, taratibu, miongozo na mazingira ya biashara mifugo na mazao yake;*<br>*2. Kuimarisha uwezo wa taasisi na mifumo ya taarifa kwa ajili ya maendeleo na usimamizi wa sekta wa mifugo;*<br><br>*(Na.2 hadi 10 ya ASDP) ambazo ni:*<br>*3. Kuimarisha miundo na uwezo wa kitalaam wa vikundi vya wakulima na/ au vyama vya wazalishaji, wafanyabiashara, na wasindikaji wadogo;*<br>*4. Kuanzisha na kuendeleza ushiriki wa makundi/jinsia tofauti kwenye sekta ya Kilimo;*<br>*5. Kuimarisha uratibu wa sekta katika ngazi zote za utekelezaji*<br>*6. Kuwezesha upatikanaji na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa takwimu katika sekta ya kilimo;*<br>*7. Kuimarisha uwezo na mifumo ya uongozi katika sekta ya kilimo;*<br>*8. Kuandaa na kuimarisha Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini;*<br>*9. Kuwezesha na kuimarisha uwezo wa utendaji wa shughuli za kilimo kwa watendaji wa sekta ya kilimo katika ngazi zote;*<br>*10. Kuimarisha mifumo ya kiteknolojia ya habari na mawasiliano katika sekta ya kilimo (TEHAMA);*<br>*11. Kutoa na kuwezesha huduma za kifedha (daraja la kawaida katika kuendeleza shughuli za kilimo (provide microfinance services.* |